

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda)

MANISPAA MPANDA

Telegraphic "REGCOM"

Simu Na. 025 – 252957128

Nukushi Na. 025 - 252957129

Baruapepe:mpandamc@go.tz

www.mpandamc go.tz.

Unapojibu Tafadhali taja:



Ofisi ya Mkurugenzi,
Halmashauri ya Manispaa,
S. L. P. 216,
MPANDA.

Kumb. Na. KTV/MMC/A.40/2/47

04/05/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi **24** za **Watendaji wa Vijiji III.**

1. SIFA ZA MWOMBAJI

I. Mtendaji wa Kijiji III

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha **IV/VI** wenye cheti/Astahada **NTA Level 5** katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

2. MSHAHARA

Mshahara utanzia Ngazi ya **TGS B.**

3. MAJUKUMU YA KAZI

- I. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- II. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- III. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- IV. Utaratibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji
- V. Kutasfiri na kusimamia Sera, Sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali Kijiji
- VI. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- VII. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- VIII. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji

- IX. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji
- X. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi.
- XI. Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji na
- XII. Atawajibika kwa Mtendaji wa kata.

MASHARTI YA JUMLA

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
2. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
3. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na Wamejipatia sifa za kuingilia katika kada tofauti walizonazo, wapitishie barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
4. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (**Detailed CV**) yenye anuani na namba za **simu za kuaminika** pamoja na majina ya wadhamini watatu (3) wa kuaminika.
5. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya kidato cha nne au sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia kazi husika. Pia iambatishwe picha ndogo (passport size) ya hivi karibuni na iandikwe jina nyuma yake.
6. Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form VI and form IV result slips) **HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na mamlaka husika (**NECTA, NACTE** na **TCU**).
8. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
9. Uwasilishaji wa sifa za **kughushi** wahusika watachukuliwa hatua Stahiki za kisheria.
10. Maombi yaandikwe kwa mkono na muombaji kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.
11. Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano.

Maombi yote yatumwe kupitia anuani ya posta kama ifuatavyo:

Mkurugenzi wa Manispaa,
Manispaa ya Mpanda,
S.L.P 216,
MPANDA.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/05/2020 saa 9.30 Alasiri.

Limetolewa na



Michael F. Nzyungu
MKURUGENZI WA MANISPAA
MPANDA.

MKURUGENZI WA MANISPAA
MANISPAA YA MPANDA
S.L.P. 216
MPANDA-KATAVI

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye :

1. Tovuti ya Halmashauri ya Manispaa – www.mpandamc.go.tz
2. Tovuti ya Secretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma www.Ajira.go.tz